Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na (kumbukeni). Tulipofunga ahadi na wana wa Israeli: Hamtamwabudu ye yote ila Allah; na mwafanyie wema wazazi na jamaa na mayatima na maskini; na semeni na watu kwa wema na simamisheni Sala na toeni Zaka; kisha mkakengeuka isipokuwa wachache tu katika ninyi na mwaenda upande.(Al-Baqara 2:84)

JUZU 79 No. 206 | SHAW. - DH. QA'D 1439 AH | JULAI 2019 | WAFA 1398 HS | BEI TSH. 500/=

Chimbuko la Msukosuko Duniani ni

Vita vya Kibiashara

Na **Mwandishi Wetu**

Mataifa yamo katika vita nyingine, safari hii vinaitwa vita vya biashara. Sio tu na majirani bali na nchi nyingine pia. Mapambano haya ya kibiashara yanaongezeka na kuenea hivyo kuongeza wasiwasi duniani kote.

Merikani chini ya utawala wa Trump ndiyo taifa linaloongoza katika vita hiyo ya kibiashara dhidi ya China, Umoja wa Ulaya, Mexiko na Kanada.

Hivi karibuni Merikani imeifutia mbali kibali kampuni ta Kichina Huawei inayohusika na mambo ya mawasiliano kwa kisingizio cha maswali ya usalama - jambo ambalo linaleta mtikisiko duniani.



Wachunguzi wa mambo wanaona mwendo huu kuwa si tu unatishia amani ya dunia lakini wanasema inaweza kuwa na athari kubwa kwa uchumi wa Merikani katika siku za baadaye.

Katika mnasaba huu, nchi wahanga zimeitelekeza Merikani na kufanya makubaliano ya biashara na nchi nyingine. Kwa mathalan, Kampuni ya Kichina ya Huawei imewekeana mkataba wa kibiashara na kampuni ya mawasiliano ya Urusi ili kuhimili marufuku iliyowekwa na uongozi wa Trump. Zaidi ya hayo, wametangaza kuwa wameandaa mfumo wa uendeshaji wa kwao pia.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu wa Uingereza Theresa May amejiuzulu kutoka kwenye uongozi wa chama chake kufuatia kukosa

Endelea uk. 2

Ansarullah Wafanya Maonyesho ya Vitabu Masjid Salaam

Na Ally Khamis Mbambwa, Sadr Ansarullah Tanzania

Majlis Ansarullah iliandaa Maonyesho ya vitabu ya wazi mbele ya Msikiti wa Masjid Salaam uliopo Makao Makuu ya Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Dar es Salaam Tanzania.

Madhumuni ya maonyesho hayo ni kufikisha ujumbe wa Islam na Masih[as].

Pamoja na kuonesha vitabu mbalimbali vya mafundisho ya dini, kulikuwa na picha kubwa ya Masihi Aliyeahidiwa[as] ambayo ilikuwa ni kivutio kikubwa katika maonyesho hayo, ambapo baadhi ya watu waliipiga Picha na yaliulizwa maswali mengi kuhusu Picha hiyo.

Pia kulikuwa na Bango zenye hoja mbalimbali ambazo Nazo ziliwavutia wengi kama vile Hoja za



i) Utume unaendelea

ii) Nabii Isa[as] Amefariki

iii) Yesu hakufa Msalabani na nyingine nyingi.

Katika maonyesho hayo ambayo yamefanyika kwa siku nane mfululizo toka tarehe 21-28 June 2019; Vitabu mbalimbali viliuzwa na vipeperushi 5,500 vilisambazwa huku Takriban watu 10,200 walifikishiwa ujumbe.

Katika maonesho hayo, mijadala iliyotia fora ni juu ya Utume kuendelea, kifo cha Nabii Isa[as] na Kufika kwa Imam Mahd na Masih Aliyeahidiwa[as].

Bwana Abdulrahman Kiwanga ambaye anatoka chama cha Mabaharia nchini, amevutiwa na maonesho yetu na akasifu mipango ya Jumuiya ya kufikishia watu ujumbe wa dini kiasi hiki amepata shauku ya kujiunga,

Endelea uk. 8

Njia Pekee ya Kuungana na Allah ni Ibaadat uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Ni Utandawazi au Utandawizi?

Dhana ya utandawazi imeibua hisia kali miongoni mwa wasomi, watafiti na wafuatiliaji wa masuala ya kimataifa. Wapo wanaosema utandawazi ni hatua ya juu katika ustaarabu na maendeleo ya binadamu kwani dunia sasa ni kijiji kilichojengeka katika kanuni kuwa binadamu wote ni sawa na wote wanastahili kufaidika na maendeleo yaliyopatikana duniani. Wengine kwa hisia kali na kwa mishipa kuwatoka utandawazi wao si chochote bali ni utandawizi.

Utandawazi ni ukoloni kwa kupitia mgongo wa nyuma na wa hadaa. Sasa hivi vyombo vya magharibi, mabunge, vinazungumzia demokrasia isiyo na mipaka, uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kufanya biashara. Dunia ni kijiji cha watu walio sawa na wanaoshirikiana kufanya dunia hii kuwa mahali pazuri pa kuishi.

Huu ni mwendeleo wa sera za hadaa. Ni kweli dunia hii ni kijiji. Tunawasiliana. Tunafanya biashara. Swali la kujiuliza katika kijiji hiki tuko sawa au tumegawanyika katika matabaka ya wale ambao wanaambiwa tufanye biashara lakini hawana cha kuuza! Wanaambiwa tufanye biashara lakini bei wanapanga wao! Wanapozungumzia demokrasia wana maana ya maslahi yao watetezi hao wa haki za binadamu. Mwandishi wa habari anaumwa lakini wanakuwa kimya kwani wana silaha za kuuza. Baadhi ya mataifa yalilindwa kutengeneza silaha hatari, kwa wengine mwiko.

Katika kijiji hiki uko wapi uadilifu? Khalifatul Masih wa V*atba* amekuwa akipigia kelele ukosefu huu wa uadilifu katika mabunge ya Ulaya, Uingereza na Merikani. Nchi masikini zinaonewa na kunyonywa. Hali hii inahatarisha amani na inazidi kujenga hofu.

Utandawazi wa kweli umeletwa na Islam. Kwa Islam haki za binadamu hazitolewi na bunge, Mfalme au kiongozi. Haki hizo Amezitoa Allah. Allah Anasema katika Qur'an Tukufu kwamba kumuua mtu mmoja ni kama umeuwa dunia nzima. Kuhakikisha maisha ya mtu ni sera ya msingi ya Islam. Islam inataka mali itawanywe kwa wote. Masikini huwasaidii bali kuna haki yao katika mali yako. Islam inasema binadamu wote wameumbwa sawa na Allah Anasema mbora wenu si kwa sababu ya rangi isipokuwa uchamungu.

Tunaikaribisha dunia iingie katika nyuma hii salama ya utandawazi iliyojengwa na matofali ya Islam. Nyumba yoyote nyingine haitakuwa nyumba bali itajizolea sifa ya nyumba ya Ankabuti – moja ya nyumba dhaifu duniani.

Vita vya Kibiashara na Msukosuko wa Dunia

Kutoka uk. 1

kuungwa mkono kwa wabunge wake kuhusu Uingereza kujitoa katika Umoja wa Ulaya katika sehemu ngumu na kuacha mgawanyiko mkubwa kuliko ule kabla hajawa Waziri Mkuu. Sasa hivi kuna mbio za kisiasa za nani atakayerithi mikoba ya Bi. Theresa.

Mataifa yanajitahidi kulinda maslahi ya mataifa yao na kufuata sera ya Mwombe-Jirani-Yako ambayo italeta maafa makubwa. Kiongozi wa Ahmadiyya duniani Hadhrat Mirza Masroor Ahmad atba kwa kutafakari juu ya hali hii, amesema:

"Kwa matamshi ya mdomoni ni rahisi kusema unamtakia kila la kheri jirani yako, lakini kwa hali halisi hilo ni jambo gumu na ni mtihani panapokuwepo na mgongano wa maslahi, mara nyingi mtu anafikiria upande wake bila kujali haki za wengine" (Mhadhara, Chuo Kikuu cha York,Toronto 28 Oktoba 2016).



Vipeperushi vya Zuia Vita Kuu ya Tatu ya Dunia vilivyoandaliwa na Jamat ya Uingereza na kusambazawa mitaani

Wanachama wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya hivi karibuni walikusanyika mbele ya bunge ili kuwatanabahisha watu wa Uingereza haja ya uadilifu ili kuepukana na vita ya III.

Katika mnasaba mwingine Khalifatul Masih wa V atba anasema, "uzito wa unyeti wa hali hii ya vita ya tatu nikanakwamba inaweza kutokea wakati wowote - kwa hakika, kwa uhalisia, vita ya tatu imekweisha anza ingawaje kwa hali ndogo. Nimekuwa nikionya hili kwa miaka mingi na sasa wachambuzi wa mambo na viongozi wa dunia wameanza kumaizi na kukubali" (*Hotuba ya Ijumaa, Baitul Futuh, 4 Disemba 2015*).

Nchi zenye nguvu duniani na nchi zilizo imara lazima waone mawimbi haya katika dunia na wazingatie maslahi ya nchi zenye nguvu haba ili sasa waweze kupanda mbegu ya amani na maelewano duniani. Mataifa yajitahidi kujenga haki hata kama ni kwa kujitolea muhanga kuhusu maslahi yao.

Ijtimaa ya Lajna Imaillah Yanoga



Na **Idara ya Ishaat**
Lajna Imaillah - Tanzania

Ijtimaa ilikua na watu zaidi ya 600 Watu wengi walijitokeza kushiriki mwaka huu kuliko miaka mingine ikapelekea changamoto kwa majudge katika ugawaji wa zawadi na katika kukamilisha zoezi zima. Mikoa iliyoshiriki ni 13. Khuddam na Ansar hawakua nyuma kuhakikisha Ijtimaa yetu inafana. Tulipata msaada wa kutosha. Atfal nao hawakukubali kuwa nyuma. Shura nayo ilikua nzuri, wajumbe wenye weledi walihudhuria. Tulipata madarsa mbalimbali kama vile ya Quran na Masharti ya biat, afya, nk. Chakula kilikuwa motomoto.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Imam Fakhruddin Razi



Na

Mwl Abdullah

Hamis

Mbanga,

Redio Ahmadiyya,

Mtwara

Kutoka toleo lililopita

UMUHIMU WA IMAM RAZI

Imekwishaelezwa kabla kwamba kazi za Imam Razi zimezifunika zote za watangulizi wake katika fani za dini na dunia, hasa katika ufasaha wa lugha, wepesi wa maelezo na urahisi wa kukumbukwa. Baada ya Imam Ghazali, Imam Razi anasimama kama ndiye bingwa aliyeoanisha ufahamu na ufunuo kwa misingi ya hoja za kiakili. Amejaribu kutoa suluhisho katika masuala yote magumu kwa kutumia ufahamu wa kiakili. Katika jitihada zake hizo, anaeleza katika kitabu chake maarufu kabisa *Tafsiirul Kabiir* kwamba, Kurani tukufu ina kila aina ya elimu na anajadili maswali mazito kabisa ya kifalsafa kwa maelezo ya aya za Qur'an. Akiwa mwenye mitazamo huru, mara kwa mara ananukuu beti za mwanafalsafa mshairi, Abul 'Alaa Al Ma'arri kuthibitisha nadharia zake katika vitabu vyake vingi.

Baada ya kusoma vitabu vya Abu Ali bin Sina na Abu Nasr Muhammad Al Farabi, Imam Razi alikuwa bingwa wa theolojia na elimu mbalimbali kiasi cha kukosa mpinzani katika zama zake. Akiwa kama mtetezi mkuu wa Sunni, alifanya mijadala mingi na wanazuoni wa madhehebu mengine ambapo aliwaangusha vibaya katika uwanja wa hoja. Hoja zake za kimantiki ziliwafanya wapinzani wake wengi wajiunge na Ahlus Sunna baada ya kujadiliana naye. Imam Razi pia alikuwa mmoja wa wakosoaji wakubwa. Ukosoaji wake haukwaacha salama hata maimamu wakubwa waliomtangulia kama; Abul Hasan Ash'ari, Abu Bakr Muhammad Ibn Furak, Qadhi Abu Bakr ibn Arabi na Imamul Haramain. Hawa na wengine wengi alikosoa baadhi ya mafundisho yao.

Kuelekea mwishoni mwa maisha yake alipokuwa amefikia katika kilele cha elimu yake, alikumbwa na dhana ileile iliyowahi kumkumba Imam Ghazali hapo zamani. Kujiamini kwake juu ya ufahamu wa mwanadamu kulipata mtikisiko. Yawezekana kutokana na zile dhana za kisufi za Sheikh Najmud din, Imam Razi alikuwa akihubiri misimamo tofauti kuhusiana na elimu na ufahamu. Alionekana kutoyashangilia sana matumizi ya hoja za kiakili katika kuutafuta ukweli. Dhana aliyoihubiri, kuitumia na kuiandika katika maisha yake yote, sasa alikuwa akizikejeli katika beti kama hizi zifuatazo;

Nihaayat iqdaamil 'uquuli 'uqaalu, wa aktharu sa'al 'alamiina dhwalaalu. Wa arwaahinaa fii wahshati min jusuuminaa, wa haaswil duniyaana radyanw wa wibaalu. Wa lam nastafda min bahithnaa twuulu dahrinaa, sawaa an jama'na fiihi qultu wa qaaluu. Wa kam qad ra-ainaa min rijaalinw wa daulah, fabaaduu jami'am musri'iina wa zaaluu.

Wa kam min jibaali qad 'allat sharafaatuhaa, wa 'aala fazaalat wal jibaalu jabaalun.

Mwisho wa utangulizi wa akili ni pingu, na mengi wayaendeayo walimwengu hupotea. Na roho zetu hutishwa na miili yetu, na chumo la dunia yetu ni maumivu na uasi.

Wala hatufaidiki na mijadala ya maisha yote, ni sawa na kukusanya tu nilichosema na walichosema.

Wangapi tumewaona katika watu na mataifa, wote waliharakia kujimaliza na wakaenda. Ni milima mingapi ilyokanyagwa na watu, nao wakaondoka milima ikabaki.

KIFO CHAKE

Ikumbukwe kwamba Imam Razi hakuwa mhubiri na mwalimu tu, lakini pia alikuwa bingwa wa mijadala. Uwezo wake wa kuvunja hoja za wengine, pamoja na ujasiri, kujiamini, lugha kali na jazba, vilimjengea idadi kubwa ya maadui. Mafanikio yake ya kimaisha yaliwafanya wengine wamuonee wivu.

Kuna wakati aliweza kuonyesha hali ya kutojali, mathalan akiwa katika kilele cha umaarufu, kaka yake, aliyepinga maendeleo yake hadharani, alifungwa na Khwarazm – Shah (Mtawala wa Turkistan) na akafia jela. Aliwahi kugombana na mhubiri mmoja maarufu, kisha mhubiri huyo akazamishwa baharini kwa amri ya ufalme. Aliwahi kufutilia mbali hoja za Waismailia juu ya uhalali wa Imam wao wa saba, hata wakafikia hatua ya kumpelekea jasusi aliyetishia kumdunga kisu. Na juu ya yote aliwabana sana kwa hoja wafuasi wa kundi la Karramiyyah. Inasemekana kwamba hata kupigwa kwao marufuku kulitokana na Sultani kuvutiwa na hoja za Imam Razi. Katika hali hii Imam Razi alijikuta akiwa mlengwa wa mengi ya maadui zake. Imewahi kuelezwa kuwa hata kifo chake hakikutokana na sababu za kawaida, bali inadaiwa kuwa alipewa sumu na wafuasi wa kundi la Karramiyah, ikiwa ni hatua ya kulipiza kisasi kutokana na walichokiita uadu wake dhidi yao.

Wafuasi wa kundi hili hawakumwacha huru Imam Razi. Kila walipopata nafasi ya kumshambulia au kumdhuru waliichangamkia na kuitumia vilivyo. Walikuwa wakizomea, wakimtukana na kumshambulia kila walipopata wasaa naye. Kuna wakati waliwahi kumvurumishia mawe mimbarini alipokuwa akitoa hotuba kwa ufasaha mkubwa. Ni katika tukio hili la kusikitisha ndipo alikariri ubeti huu akiwa juu ya mimbari kwamba; ***Al mar-u maa daama hayya yastahaanu bihi, wa yu'dhamur ruz-u fiihi hiina yaftaqid. Mwanadamu maadamu yu hai hupuuzwa, na hubainika msiba mkubwa pale atowekapo.***

Kama tulivyokwishaeleza kwamba Karramiyya walimtuhumu Imam Razi kuwa ndiye aliyehusika na kifo cha mtu wao wa muhimu, Sultan Shihabud din Al Ghuri. Na hili hawakulisahau, siku zote walikuwa wakitafuta upenyo wa kummaliza. Hatimaye walifanikiwa kumkodi mtu aliyefanikiwa kumpa sumu Imam Razi kupitia kinywaji. Aliweka sumu kwa siri katika sharubati, kisha akampatia Imam Razi. Alipokunywa athari za sumu zilipelekea Imam Razi kupoteza maisha. Alifariki mnamo machi 29, mwaka 1210, mjini Herat, Afghanistan akiwa na umri wa miaka 61.

VITABU VYAKE

Imam Razi ametuachia idadi kubwa ya vitabu, kazi zake nyingi zilipata umaarufu mkubwa tangu zama za uhai wake. Ukiachana na ile kazi yake maarufu kabisa ya tafsiri ya Kurani Tukufu, *Mafaatihul Ghaib* ambayo hujulikana sana kama *Tafsiirul Kabiir*, pia ameandika vitabu vingine vingi. Inaaminika kuwa Imam Razi alipata kutunga vitabu, vikubwa na vidogo zaidi ya mia moja katika maisha yake. Uandishi wake ulijikita katika fani mbalimbali kama vile, tafsiri, theolojia, falsafa, fikia, metafizikia(Metaphysics), usuul n.k.

Baadhi ya vitabu vyake vingine ni kama vile; *'Ajaaibul Qur an* (Maajabu ya Kurani), *Al Mahsul fi 'ilmul Usuul*, *Mawaakif fi 'ilmil kalaam*, *'Ilm al Alhlaq*, *Kitaabul Firasa*, *Kitabun Nafs war ruh*, *Mataalibul 'Aliyah*, *Risala Al Huduth* na vingine vingi.

Kupitia uandishi wake, Imam Razi ndiye aliyefafanua kwa kina dhana ya kuwapo kwa ulimwengu zaidi ya mmoja (Multiverse). Katika kitabu chake *Mataalibul 'Aliyah*, Razi anakosoa dhana ya kale na maafu mno ya wanajiografia na wanajimu ya kwamba kuna ulimwengu mmoja tu, na hivyo kusisitiza dhana mpya kuwapo kwa ulimwengu zaidi wa huu tulio nao katika Galaksi hili la jua letu. Dhana hii bila shaka aliiendeleza kutokana na tafsiri yake juu ya aya Suratul Faatiha, ***Alhamdulillahi Rabbil 'alamiin*** ambapo aliibua hoja kwamba neno 'alamiin liko katika sigha ya wingi, hivyo inamaanisha kwamba kuna tabaka kadha za ulimwengu katika anga (*cosmos*). Akifafanua hili katika kitabu chake *Mataalibul 'Aliya* anasema;

Inathibitika kutokana na ushahidi kwamba nje ya ulimwengu kuna ombwe lisilo na mwisho Khala' laa nihaayatanl laha, na pia imebainika kwa ushahidi wa kutosha kwamba Allah S.W. Ndiye Mwenye uwezo na umiliki juu vyote hivyo. Na hivyo Yeye ni *Qaadirun 'alaa any yakhluqu alfa alfi 'awaalim* - Mwenye uweza wa kuumba Maelfu elfu ya ulimwengu nje ya ulimwengu wote (Alfa alfi humaanisha milioni) na kwamba kila ulimwengu huko ni mkubwa kuliko huu tulio nao. Na una kila kitu kilichomo katika ulimwengu huu kama vile arsh, kursiyy, samawat, al ardh, ash shamsu wal qamar. Kwa hoja hii alithibitisha udhaifu wa dhana ya wanafalsafa wa zama zile kwamba ulimwengu ni mmoja tu. Dhana ya ulimwengu mmoja (single universe) ilikuwa ndiyo dhana ya Aristole, Euclid, Plato na wanafalsafa wengi wa Kigiriki. Hata Abu Ali bin Sina naye alishika dhana hii hii.

Dhana hii imejadiliwa kwa kina katika jalada la 5 la kitabu hicho. Humo amejadili pia uwepo wa eneo tupu (vacum) nje ya ulimwengu ambalo Allah Anaweza kulijaza kwa ulimwengu mwingi mwingine.

Dhana hii ambayo Imam Fakhrud din Razi alikuwa akiizungumzia zama hizo mnamo karne ya tisa, leo hii katika karne ya 21 bado ni habari mpya inayoendelea kusisimua hamu za watafiti wa kisayansi kila uchao. Bila shaka Imam Razi amefariki zaidi ya karne kumi zilizopita, lakini mawazo na kazi zake zinaishi hata sasa. Allah Awe radhi naye na Atunufaishe kwa elimu yake. Amin

Ibaadat - Njia ya Kuungana na Allah

Asema Khalifatul Masih wa V^atba



Khuddam na Atfal katika kikao cha mwisho cha ufungaji wa Ijtimaa

Kwa msaada wa Allah kuanzia tarehe 14-16/06/2019 Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ilifanikiwa kufanya ijtmaa yake ya 30. Katika viwanja vya Ahmadiyya kitonga, Ilala Dar es Salaam.

Khuddam na Atfal walisafiri kutoka katika sehemu mbalimbali za Tanzania bara na Zanzibar kuja katika mkusanyiko huu mkubwa wa vijana wa Kiislamu Ahmadiyya. Kwa fadhila za Allah mwaka huu Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania tulipata bahati kubwa ya kutumiwa kauli mbiu ambayo ni ***Ibaadat*** na ujumbe maalumu na Khalifa tul Masihi V. Hadharat Mirza Masroor Ahmad*atba*. Kauli mbiu hiyo ya mwaka ya ***ibaadat*** ilibeba maudhui mazima ya nini kinachohitajika kwa kijana wa Kiislamu ili kupata maendeleo ya kweli na kushika kiini na mzizi wa mafundisho sahihi ya dini tukufu ya Islam. Kila mshiriki wa Ijtmaa hiyo alitakiwa kutafakari kwa kina zaidi maana hasa ya ***ibaadat*** pamoja na ujumbe aliotutumia Huzur*atba* Ujumbe ulisomwa kwa siku zote tatu ambazo Ijtimaa ilikuwa ikiendelea. Kwa hakika kila aliyesikiliza ujumbe huo aliweza kupata athari ya mapinduzi ya khulka kwani Huzur*atba* alitoa dira ya maisha kwa Khuddam na Atfal wa Tanzania.

Ujumbe wa Huzur*atba* uligusia zaidi maana hasa ya kalima na falsafa yake. Huzur Anwar alisema kuwa kila kinaja wa Kiahmadiyya anatakiwa kuweka kipaumbele maana hasa ya ***"Laailaahallallaah Muhammadur Rasuulullaah"*** Hapana Mola Apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na Muhammad*s.a.w* ni Mtume Wake.

Huzur Aqdas alisema sehemu ya kwanza ya Kalima ***Laailaahallallaah*** ni kanuni ya kwanza ya kuzingatia katika maisha ya kila Muislam ni kuishi Maisha ya Tauhid. Maudhui ya jumla na yalivyokubaliwa ni kwamba Allah ni Mmoja na Hana mshirika.

Aliendelea kwa kusema haitoshi kusema maneno hayo bali ni lazima yaambatane na dhihirisho la kiimani na dhihirisho hilo ni kumuabudu Allah na njia kuu ya kumuabudu Allah ni kupitia sala.

Huzur*atba* alisema sehemu ya pili ya Kalima ni ***Muhammadur - Rasuulullaah*** kwamba Muhammad (saw) ni Mtume wa Allah. Alisema mtukufu Mtume*saw* ni mfano bora kwa watu wote ni lazima kuyaishi maisha yake kwani aliweza Kutekeleza maamrisho yote ya Allah kwa kiwango cha juu sana. Kwa hiyo kila kijana wa Kiahmadiyya ana wajibu wa kuyaiga maisha ya Mtume*saw* kwa kipawa alichojaliwa na Allah kwa kufanya hivyo tutakuwa tumemfuata Mtume saw. Huzur Anwar alisisitiza zaidi kwa kusema vijana wetu ni lazima watambue thamani ya dhahabu hii, kwa njia hiyo tutakuwa tumepata kufungua mafanikio.

Huzur alimalizia ujumbe wake kwa kututaka Khuddam na Atfal kuzikimbilia fadhila hizi kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeungana na Allah kusimamisha ibada kutaleta marekebisho ya kitabia kwa kuwaonesha wasio Waislamu kuwa Islam ndio njia sahihi ya kumfikia Mwenyezi Mungu.

Ijtmaa ya mwaka huu ilipambwa na ratiba iliyoanza na khutuba ya ufunguzi iliyotolewa na Maulana Sheikh Bakri Abed Kaluta – Naib Amir Tarbiyyat na Tabligh. Naibu Amir alisisitiza kuzingatia ujumbe wa Huzur Anwar. Katika kuhakiki Ijtmaa inakwenda vyema Sadr Majlis, Bwana Ramadhani Nauja alisema kila mshiriki ana wajibu mkubwa wa kushiriki kila shindano katika mashindano yaliyoainishwa ikiwamo mashindano ya kielimu, kimwili, kwani kwa kufanya hivi tutakuwa tumeuenzi Ukhalifa. Mipango yote hii imepata ridhaa ya Khalifa wa zama. Sadr sahib alisema mipango hii imewekwa ili kukuza viwango vyetu vya uchamungu na sio tumekuja kumtafuta mshindi katika mashindano haya.

Ijtimaa ya mwaka huu ilipata baraka ya kufungwa na hotuba iliyotolewa na Amir na Mbashiri mkuu Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudry. Amir sahib alisema kuwa ni lazima kuzingatia kila Khuddam kuwa nyinyi ndio uti wa mgongo wa Jamaat itakuwa ni uti wa mgongo kama mtakuwa mbele katika kila mpango utakaowekwa iwe wa Mahubiri au malezi na mingineyo. Aliendelea kwa kusema ili muwe Khaddim na Twifl wa kweli ni lazima kutilia maanani kwa kiwango cha juu jambo hilo. Amir sahib alimaliza kwa kuiombea mafanikio makubwa Ijtimaa hiyo.

Kwa fadhila za Allah Ijtmaa ilihudhuriwa na wajumbe zaidi ya 500. Ilipata uwakilishi wa mjumbe aliyemuwakilisha Sadr wa Uganda. Bwana Ahmadi Kasimu. Pia wajumbe waliweza kuchangia chupa za damu kwa benki ya taifa ya damu salama zaidi ya 50.



Ijtimaa ya 6 ya Atfal iliendelea sambamba na Ijtimaa ya 30 ya Khuddam

TANGAZO LA JALSA SALANA TANZANIA YA 50 MWAKA 2019

Amir na Mbashiri Mkuu nchini anapenda kuwaarifu Wanajumuiya wote kwamba, Jalsa Salana ya Kitaifa mwaka huu itafanyika siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili tarehe 27, 28 na 29 Novemba 2019, katika eneo la Jumuiya, Kitonga Dar es Salaam. Inshaallah. Hivyo tunatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Wanajumuiya wote wajitahidi kuhudhuria Jalsa hiyo na ihakikishwe kwamba kusiwepo hata tawi moja katika kila mkoa ambalo halitokuwa na angalau mtu mmoja atakayehudhuria Jalsa.

2. Masheikh na walimu wajitahidi sana kuwakumbusha wanajuiya juu ya umuhimu na baraka za kushiriki kwenye Jalsa Salana kwa nauli zao wenyewe. Pia kwa vile wanajumuiya wa mkoa wa Dar es Salaam kimsingi hawahitaji nauli ikilinganishwa na wale wa mikoani basi wote wasikose kuhudhuria Jalsa hiyo.

3. Marais wa mikoa na viongozi wengine wa Majlis za matawi nao wajitahidi kuhudhuria Jalsa Salana kwa nauli zao.

JALSA SALANA TANZANIA MUBARAK

Mkutano wa Mwaka wa Kwanza, Disemba 1891



Sheikh Muzaffar Durrani
Rabwah, Pakistan

Seyyidna Ahmad[as] Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya akitoa madai kuhusu kifo cha Nabii Isa[as] Aliandika

"Naapa kwa jina la Allah kwamba madaiyanguyakuwaMasihiMau'udi ni ya kweli kama yalivyokuwa ya kweli madai ya Unabii na Utume ya Manabii wengine. Msingi wa madai haya ni kwamba kwa miezi kadhaa mfululizo nilifunuliwa kwamba Masihi mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu ameshafariki, na Masihi Mau'udi aliyetabiriwa kuja ndiye wewe. Niliambiwa, nilifahamishwa mfululizo kwa kashfi, kwa ufunuo na kwa ruya, hata hivyo sikuwa na yakini. Lakini, baada ya miezi kadhaa jambo hilo lilipofikia daraja la mfululizo, yakini kamili na yakini ya haki, ndipo nilifungua Qur'an Tukufu na nikafikiri kwamba inapaswa nilinganishe ufunuo wangu kwa Kitabu cha Allah. Kwa kufungua tu Qur'an Tukufu, aya ya Suratul Maaida *falamma tawaffaitani* ikatokea. Nilipoitafakari, nilizikuta funuo, kashfi na ruya zangu kuwa sahihi, na ikawa wazi kwangu, na ikathibitika kwamba bila shaka Masihi mwana wa Mariamu[as] ameshafariki. Kisha nikaisoma Qurani Tukufu kutoka mwanzo mpaka mwisho kwa makini na kutafakari sana, basi ukapatikana uthibitisho wa kifo cha Masihi[as], na haukupatikana uthibitisho wowote wa uhai wa Masihi[as] Kisha nikafungua ***Sahihi Bukhari***. Ni kudra ya Mungu, nilipofungua tu mara zikatokea aya mbili za Kitabut Tafsir, moja ilikuwa *inni mutawaffika* na ya pili *falamma tawaffaitani*. Tafsiri ya moja *mumituka* ilikuwa imetolewa na Ibnu Abbas[ra], na tafsiri ya pili ilifanywa na Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe. Kana kwamba Imam Bukhari alidhihirisha itikadi yake kwa kujumuisha pamoja aya mbili zilizopo katika sehemu tofauti, kwamba kwa aya hizo mbili kifo cha Masihi[as] kinathibitika na hakuna kitu kingine. Kisha nikasoma ***Sahihi Bukhari*** nzima neno kwa neno kutoka mwanzo mpaka mwisho, humo pia sikukuta neno lolote la uhai hata kwa ishara au kwa kinaya, isipokuwa kifo tu. Kisha nikasoma neno kwa neno ***Sahihi Muslim*** na vitabu vingine vyote vya Hadithi na kwa makini sana nilisoma kila mstari na kila herufi, lakini sikukuta uhai wa Masihi[as] isipokuwa mauti. Naam, Hadithi kuhusu nuzuul kushuka zinazotajwa, haimo huko 'kushuka kutoka mbinguni'. Ushukaji na uhai unahusikaje? Wakati ambapo kuwa hai na kunyanyuliwa mbinguni hakuthibitiki, basi kushukuka kuna maana gani? Msafiri pia anaitwa katika Kiarabu naziil, mshukaji, kama vile nimeshuka sasa katika Delhi." (***Hayati Ahmad*** J. 3 uk. 182-183)

Siku za baada ya madai ya Umasihi zilikuwa za shughuli nyingi sana kwa Hudhur[as]. Maulamaa wapinzani waliwasha moto wa upinzani pande zote nne, lakini Hudhur[as] kwa heshima kubwa alikuwa ameshughulikia kwa uimara na ushujaa akizima moto huo, na kwa lengo hilo akafanya pia safari ndefu ndefu. Lakini pamoja na kusimama vitani mwa itikadi kwa upanga uliochomolewa, hakughafilika pia na malezi ya watu wapya wafanyao baiati. Basi, kwa agizo la Allah, Hudhur[as] aliweka msingi wa mkutano wa mwaka katika Qadian. Hivyo, mkutano wa kwanza wa siku moja tu, uliofanyika tarehe 27 Desemba 1891, watu sabini na watano walishiriki. Na kwa lengo na makusudio ya mkutano, alitoa tangazo tarehe 30 Desemba 1891 kama ifuatavyo:

"Ndugu wote wenye ikhlasi waliofanya bai'ati yangu wajue kuwa shabaha ya kufanya bai'ati ni kwamba mapenzi ya dunia yapoe, na mapenzi ya Mola Mtukufu na ya Mtume Mtukufusaw yatawale moyoni. Na hali ile ya kutengana na dunia ipatikane ambayo kwayo safari ya Akhera isionekane yenye kuchukiza. Lakini kwa kulipata lengo hili yamlazimu mtu kukaa nami na kutumia muda fulani wa umri wake katika njia hii ili, Allah Akipenda, kwa kushuhudia dalili yenye yakini, udhaifu na uzembe uondoke, na kwa kuzalika yakini kamili izalike shauku na ladha ya jazba ya upendo mkubwa. Hivyo, kwa ajili ya jambo hili, daima inatakiwa kuwa na hadhari, na yapasa kuomba dua kuwa Allah Ajaalie uwezo huu. Na mpaka uwezo huo haujapatikana inapasa kuonana nami mara kwa mara, kwani baada ya kuingia katika silsila ya baiati, kisha kutojali kuonana, baiat kama hii haina baraka, itakuwa ni kama kufuata mazoea. Na kwa vile ni vigumu kwa kila mmoja kuja hapa akae nami kutokana na udhaifu wa asili au upungufu wa uwezo au kitalifa kirefu, au kuja mara chache kwa mwaka kuonana nami kwa kuvumilia shida kubwa, kwani hivi sasa ndani ya mioyo mingi hamna shauku nyingi kiasi kwamba waweze kuvumilia taabu kubwa na madhara mengi, kwa hiyo inaonekana inafaa zipangwe siku tatu kwa mwaka kwa ajili ya mkutano ambamo, Allah Akipenda, ndugu wote waaminio waweze kuhudhuria katika tarehe zilizopangwa, sharti wakiwa na afya na nafasi na kutokuwa na vikwazo vikubwa. Kwa maoni yangu, ni bora tarehe hizo ziwe 27, 28 na 29 za mwezi Desemba. Yaani baada ya siku ya leo hii iliyo 30 Desemba 1891, kama tarehe 27 Desemba ikifika katika uhai wetu, basi ndugu wote kadri ya wasaa wao wanapaswa wafike kwenye tarehe hiyo kwa ajili ya kusikiliza maneno ya Allah tu na kwa ajili ya kushiriki katika maombi. Na katika mkutano huo kutakuwa na shughuli za kuelezea mambo ya ukweli na maarifa ambayo ni ya lazima kwa ajili ya kuzidisha imani na yakini na maarifa. Na vile vile jamaa hao watafanyiwa maombi maalum na mwelekeo mahususi na itafanyawa bidii sawa na uwezo mbele ya Allah Mrehemevu kwamba Allah Awavutie kwake na Awakubalie kwake na Awapatie mabadiliko mema... hadi mwisho." (Tangazo hilo limechapishwa kwa kitabu "Asmani Faisala)

Mkutano huo ulifanyika katika Masjid Aqsa ya Qadian. Taarifa yake iliyoandikwa katika kitabu cha Hudhur[as] "Asmani Faisala", humo mkusanyiko huo sawa na hali ya wakati ule umeitwa "halaiki kubwa". Lakini sasa Mkutano ule ulioanzishwa kwa mikono mitakatifu ya Masihi Mtukufu, unahudhuriwa na watu maelfu wenye huba kutoka duniani kote. Mamia ya wanaojitolea kwa hiari yao wanasimamia shughuli za mkutano. Na wakati ule hauko mbali ambapo malaki ya wapendao Uahmadiyya kutoka nchi zote za dunia kwa shauku na mapenzi makubwa watashiriki katika Mkutano wa mwaka, Allah Akipenda. Na sasa Jumuiya ya nchi kadha inafanya Mkutano wa mwaka wao katika nchi zao unohudhuriwa na maelfu ya wato kila mahali.

Pe Tu Pe na Amir Sood Andanenga



Na
Mahmood Hamsin Mubiru

Ni neema ilioje kuifikia Ijumaa. Ni yaumul juma'a. Ni siku kubwa. Ni siku ya Iddi. Tumeambiwa tuache tijara. Twende msikitini. Hii ni siku muhimu na maalum sawa na imani yetu. Nabii aliumbwa siku hiyo. Na ni siku hiyo pia alitolewa humo. Na siku hiyo hiyo pia ndiyo itakua ya ufufuo. Lakini kumbuka usisahau, sala ikiisha tawanyika katika Ardhi kutafuta fadhila za Allah. Ina utamu wa ajabu riziki ile unayoitolea jasho.

Kwa kumaizi umuhimu wa siku hiyo, najitayarisha. Nakumbuka methali ya Wahaya; "obwato bwengai emo busabara kara"- 'mtumbwi wenye kasia moja lazima uondoke mapema. Kuna malipo kwa wale wanaokaa mstari wa mbele msikitini siku ya Ijumaa. Sawa na Hadith ya Mtume Muhammad[saw] anayewahi kufika msikitini na kukaa mstari wa mbele anapata thawabu ya ngamia mzima. Na anayechelewa kidogo anapata ng'ombe. Anayechelewa zaidi yeye anapata mbuzi. Anayechelewa zaidi ya hapo anapata kuku na yule anayefika wakati hotuba imeshaanza kutolewa anaambulia yai. Hivyo nafanya haraka, natengeneza vizuri ndevu zangu, sio ziondolewe zote la hasha! Natengeneza 'O'. Ninapomaliza nakata kucha na kuingia bafuni, sikusahau wembe wangu, najitengeneza vizuri, naoga. Ngua zangu zilitayarishwa toka jumatano. Nafanya hivi kwa sababu umeme wetu hauna muamana. Siku hii ya ijumaa napenda kuvaa nguo nyeupe. Ndiyo sunna ya mtukufu Mtume[saw]. ukiniona utadhani nyangenyange. Kofia yangu ya kiua nilishaiweka zamani kwenye kisado (ili kuinyoosha). Imenyooka kama tuta la viazi. Si desturi kupiga pasi kofia, utaiharibu. Lakini ukiwa kwenye basi uwe mwangalifu, vijana wa mjini wanaipenda sana kofia ya namna hiyo. Utalia. Natafuta uturi ulipo, najipulizia. Wakati huo nimekwisahawaambia ahali zangu wote wajitayarishe. habaki mtu nyumbani siku ya ijumaa. Na mwanaume ni 'kawamuna'. Ni wajibu wangu. Kila mtu ni mchungaji. Atauliza alichopewa kuchunga. Ni kweli samaki hapana shaka anakunjwa angali mbichi. Watoto sikubali asilani wabaki nyumbani siku hiyo. Labda pawepo na udhuru wa kweli. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

Matayarisho yote tayari. Kabla ya kuondoka tunafanya maombi, ili Allah atufanyie wepesi katika safari yetu. Ni patshika nguo kuchanika usafifi wa jiji hili. Nahurumia nguo zangu nyeupe na uturi. Lakini hakuna njia, la kuvunda halina ubani. Tunabanana hivyo hivyo , tunafika msikitini, msikiti ni msafi wa kuvutia , ilka watu hawajaanza kuwa wengi. Nasalimiana na hao ninaokutana nao mlangoni, maamkizi yetu ni yale yale; "assalaam alaikum warahmatullah wabarakatuh". Tunakumbatiana, zamani sana tuliachana na mambo yale ya shikamoo, chei chei, sabal, heri,..... tumejikita kwenye utamaduni wa Kiislam.

Itaendelea toleo lijalo

Bustani ya Washairi

GHOFIRA

1. Nianze kwa jina lake, Yule alietukuka.
Msadake niutake, shetani sije nifika.
Anipe baraka Zake, na mimi kutakasika
Nina tubu ninaomba, ghofira yake Rabana.

2. Katuumba kwa udongo, alama ya udhaifu.
Shetani kashika gongo, kutupeleka pachafu.
Na mabo yatwenda fyongo, tumeiacha suhufu.
Nina tubu ninaomba, ghofira yake Rabana.

3. Maovu tunayajua, na tunadumu dhambini.
Tusipopata afua, tutaingia motoni.
Twakuomba erabua, twakuomba samahani.
Nina tubu ninaomba, ghofira yake Rabana.

4. Mola wangu mepotoka, na shetani kunishika.
Moyoni nimechafuka, nahitaji safishika.
Nikifanya kuzindika, kheriyo haitafika.
Nina tubu ninaomba, ghofira yake Rabana.

5. Natubu Mola natubu, toba yangu ipokee.
Ujinga ulinisibu, bure bure nasamehe.
Kwako naja ya Habibu, swawabu uniwekee.
Nina tubu ninaomba, ghofira yake Rabana.

6. Nalia macho machozi, yanitiririka sana.
Moyo mejaa majonzi, aibu ninaiona.
Allah pekee ndo Mjuzi, undani ananiona.
Nina tubu ninaomba, ghofira yake Rabana.

7. Sabaa zimetimia, kwa mola kumlilia.
Name namalizia, msamaha kutakia.
Ndugu kuwausia, tusimuasi jalia.
Nina tubu ninaomba, ghofira yake Rabana.

Bilali Kaluta

WALIKWISHASONGA

1. Ya Rabi Taali, Mola Mjenga.
Nakutawakali, ninapotunga.
Nipange kauli, za kimalenga.
Nitongoe kweli, inonitinga.
Walokwishasonga, hawarejei.

2. Wawapi Ziuli, wa Pate Yunga.
Wenye nyuso ali, Kenya mianga.
Waloyakabili, matitimanga.
Kwa kushitaghili, kinaganaga.
Walokwishasonga, hawarejei.

3. Wawapi rijali, walo vigaga.
Wenye taamuli, zisobananga.
Tena majabali, wa mitulinga.
Ala kuli hali, walijijenga.
Walokwishasonga, hawarejei.

4. Wawapi fahali, wale nganganga.
Walotajamali, kwenye viunga.
Kwa kuwakatili, walowapinga.
Leo zao hali, zimejifunga.
Walokwishasonga, hawarejei.

5. Wako wapi nguli, wa kuzitwanga.
Mabwana Kigali, wasiolega.
Na himaya kali, walizikonga.
Matusi thaqili, yaliwazinga.
Walokwishasonga, hawarejei.

6. Wawapi liwali, na manyakanga.
Waliohimili, kujifinyanga.
Ili kubadili, yalowatinga.
Wako kwa Jalali, wametutenga.
Walokwishasonga, hawarejei.

7. Wapi wanawali, walojienga.
Kwa mapambo ghali, wakajisinga.
Walimbwende kweli, walionoga.
Waliponda mali, zikawakoga.
Walokwishasonga, hawarejei.

8. Wawapi juhali, wenye mianga.
Walo kikejeli, na kusimanga.
Na nyingi fedhuli, wakazichonga.
Mwisho idhilali, ikawapunga.
Walokwishasonga, hawarejei.

9. Ni kenda kamili, beti hatunga.
Tena bulbuli, nimezipanga.
Nataka sahali, ya kujichunga.
Nitulie tuli, nizime ngenga.
Walokwishasonga, hawarejei.

Ustadh Abdullah H. Mbanga (**Kungwi**)
Radio Ahmadiyya, Mtwara.

MAISHA PANDE MBILI

1. Kila kilicho kitamu ,Uchungu hukosekani
Katakutoa Fahamu, kukutia mashakani
Itakwisha yote hamu, Hatakula sitamani
Maisha ni pande mbili ,Ishi kwa tahadhari

2. Ishi kwa tahadhari, Maisha ni pande mbili
Yataka utafakari,kabula kata shauri
Ninge itakuja mbali , Ushakushuka Msuli
Kila kilicho kitamu, Uchungu hukosekani

3. Uchungu hukosekani , Kila kilicho kitamu
Atapinga hayawani, Mjinga aso fahamu
Au Juha mjivuni ,Mhaba sona elimu
Maisha ni pande mbili, Ishi kwa tahadhari

4. Ishi kwa tahadhari,Maisha ni pande mbili
Silinge na yako mali, Wenzio kawadhariri
Waweza lala tajiri , Ukiamka fakiri
kila kilicho kitamu , Uchungu hukosekani

5. Uchungu, Hukosekani , Kila kilicho kitamu
Hapa naweka sukani, Yatosha nilo kalamu
Anae nijua nani, Si fundi si Mtalamu
Maisha ni pande mbuli, Ishi kwa tahadhari

Bwana Nongwa
RUFIJI: PWANI

MSAFARA WA KINYONGA

1. Wakuogopwa jalali, duniya aloijenga.
Bila mawe na tofali, kaumba alivyopanga.
Muweza wa kila hali, nani atakaepinga.
Allah katandaza mwanga, wenye nuru ya miali.

2. Nimeazimu kutunga, tungo za vitandawili.
Duniya ni kama tenga, lilojazwa vitu mbali.
Bali vingi vya kuchunga, na tele vya kuskuli.
Allah katupayo mali, umaskini kuwinga.

3. Duniya ni mahali, mwenyezi ametuunga.
Na viumbe mbalimbali, sufufu ni kiwanga.
Ki Usilojua ujinga, sal sibaki jahili.
la mmoja ni swali, aulizae mjinga.

4. Mfano kama kinyonga, nianalo la kusaili.
Umbo lanipa ujinga, haijagusa akili.
Ana mwendo wa kuringa, wa madaha kweli kweli.
Hali ya kujibadili, hapo tena panitinga.

5. Mkiwa kwenye sabili, mwendo kama kajigonga.
Enda mbele aghairi, arudi nyuma aunga.
Akirejeya ya pili, unamuona asonga.
Ndipo hapo panitinga, hali ya kujibadili.

6. Khatuwa anazipanga, kwa safari ya maili.
Vivyo hivyo bila ngenga, anyata ajibadili.
Hadi anadengadenga, atakapo huwasili.
Kunyata kujibadili, ndipo panaponitinga.

7. Ipi rangiye asili, aloumbwa nayo enga.
Ni yu mwekundu wa mwili, au njano ilofunga.
Nyeusi ya kuhimili, kwa uchafu wa mchanga.
Ndipo hapo panitinga haliye huyu kinyonga.

Al Ustadh Mhenga Khamis S.S Wamwera
Kimbangulile, Mbagala Rangi Tatu.
Dar Us Salaam

UPENDO KWA UKHALIFA.

Ewe mwenye Nuru tele,Mkidhi wa kila haja
Ulo hai wa milele,Mujibu wa kila hoja
Muinua wateule,Mpandisha madaraja
Tupandie mioyoni,Upendo kwa Ukhalifa

Ukhalifa ni neema,Bada ya unabii
Ausimika karima,Kwa wale wanaotii
Kwao dini husimama,Pinzani hawahofii
Matumaini twapata, Upendo kwa Ukhalifa

Tuupende Ukhalifa, Kwa roho bila kikomo
Kwani hapendi hafifa, kwenye kilo wala kimo
Huba rahaye kufa, Hilo nakupa ni somo
Daima tuupe haki, Upendo kwa Ukhalifa

I sauti ya uhai,Ndaniye roho hushiba
Hulevya kama divai,Hudumisha unasaba
Tukuze yetu jamii, tunae mmoja baba
Tushike imara kamba,Upendo kwa Ukhalifa

Dua zetu kwa Khalifa,tuzitilie mkazo
Maombi nusu kufa, hupita bila mzozo
Tumtakie kaifa, salamu haina tozo
Tuitambue thamani, Upendo kwa Ukhalifa

Tuwe tayari jitoa,Kwa nukudi na kadiri
Dini tuweze okoa,Toka mikono hatari
Watu tuweze ongoa,Kwa mapenzi na Johari
I mbele taa yetu,Upendo kwa Ukhalifa

Tufanye usaidizi, wenye jazba na hofu
Nasi tuzipande ngazi,Kwa huba na uongofu
Tuviongozi vizazi,Viepukane na ufu
Daima uwe imara, Upendo kwa Ukhalifa.

Shunda Mshundia Wana
Morogoro.

ALIYA

Tumepokea Salamu, manyoni zina tokea
Kuwa Aziza mudhamu, Mwana amejifungua
Tena Mwana lomuhimu, wakfu wa Jumuia
Karibu wetu mgeni, mtoto wetu ALIYA

Ni baraka za kudusi , Mola ilahi rabuka
Tuna kushukuru sisi, na Saidi Mgeleka
Ilikua si rahisi, machozi kutiririka
Karibu wetu mgeni, mtoto wetu ALIYA

Yahitajika nidhamu, Mwana huyu kumleya
Sote tunalo jukumu, wazazi ndugu pamoya
Tumpatie elimu, Mola Anayoridhiya
Karibu wetu mgeni, mtoto wetu ALIYA

Muumba wangu Rabuka, Mwana huyu msitiri
Kwako mimi sina shaka, mzidishie ya kheri
Utampa nayo taka, kila aombapo zuri
Karibu wetu mgeni, mtoto wetu ALIYA

Rajabu Abasi Mkieti (Al-Wattani _Mlezi)
Lusanga Muheza Tanga

Jeshi huongezeka, Karibu katika nyumba
Aliya twafurahika, dua twazidi kuomba
Uwe mwana wa baraka, ukue Kama mgomba
Hatimaye ujiunge, kwenye jeshi la Masihi

Mhariri

RADHI

Kweli safari ya tabu, kuipata yake radhi
Kumfikia Wahabu, funga Sunna na faradhi
Ili kuchuma zabibu, ushike huno waadhi
Safai hino ni ndefu, yahitaji masurufu

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani, Dar es salaam

Upendo

Mwanaume mmoja alimuoa mwanamke mrembo. Alikuwa akimpenda sana. Siku moja mwanamke alipatwa na maradhi ya ngozi. Kidogokidogo alianza kupoteza urembo wake.

Mume alipata safari na wakati akirudi alipata ajali iliyomfanya apoteze uwezo wake wa kuona. Hata hivyo, maisha yao ya ndoa yaliendelea kama kawaida. Lakini kadiri siku zilivyosonga mbele ndivyo mke alivyoendelea kupoteza urembo wake. Kwa kuwa mume alikuwa kipofu hakulijua hilo na hivyo hakuna kilichobadilika kwenye upendo wao. Aliendelea kumpenda, na mke alimpenda sana mumewe.

Siku moja mke alifariki dunia. Ilikuwa huzuni kubwa sana kwa mume.

Baada ya kumaliza taratibu zote za maziko, mazishi na kutandua msiba, alipanga kuhama kwenye mji huo na kwenda kuishi kwenye mji mwingine.

Mtu mmoja aliposikia habari hiyo alimwendea na kumuuliza: ?Sasa utawezaje kutembea peke yako? Maana siku zote hizi mkeo alikuwa akikusaidia kukuonesha njia.?

Akajibu: Mimi si kipofu. Nilifanya ionekane hivyo kwa sababu angejua kwamba ninauona mwili wake ulivyobadilika kuwa mbaya angepata maumivu makubwa zaidi kuliko ugonjwa wake wenyewe. Alikuwa mke mwema sana. Nilitaka aendelee kuwa na furaha.

FUNZO:

Wakati fulani ni vizuri ukajifanya kipofu na kuyapuuza mapungufu ya mwenzako ili kumfanya awe mwenye furaha .

Meno huung?ata ulimi mara nyingi, lakini vinaendelea kuishi pamoja kinywani. Huo ndio moyo wa KUSAMEHEANA. Macho hayaonani, lakini yanatazama na kuona vitu kwa pamoja, hupepesa na kulia pamoja. Huo unaitwa UMOJA.

Ukiwa peke yako unaweza kuongea, lakini ukiwa pamoja na mwenzako mnaweza KUZUNGUMZA.

Ukiwa peke yako unaweza KUFURAHI, lakini ukiwa na mwenzako unaweza KUFURAHIA

Ukiwa peke yako unaweza KUTABASAMU, lakini ukiwa na mwenzako mnaweza KUCHEKA.

tazama nakumbuka kuwa Kiwembe kina ukali lakini hakiwezi kukata mti; shoka lina nguvu na imara lakini haliwezi kukata nywele hivyo vyote kiwembe na shoka vina umuhimu wake kwa mahala pake

Kila mtu ni muhimu kulingana na kusudio na lengo la uwepo wake. Usimdharau mtu yeyote kwa hali yoyote, kwa sababu huwezi kuwa yeye kwa vyovyote na pia amini kuwa upo umuhimu wa uwepo wake .

Mwenyezi Mungu atujaalie nguvu na moyo wa kusamehe, kustahimiliana na kuishi kwa umoja na upendo .

Hadithi na Zaid A. Machombe, Mabibo - DSM

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yasiyopungua ishirini (20) katika jedwali hapa chini lenye maneno ishirini na nane (28)

W	A	T	H	A	M	U	D	I	J	M	I	Z	T	I	R	Q	N	Q	Y
L	G	D	W	G	P	I	F	K	A	B	F	B	V	M	S	L	M	Q	X
T	T	L	T	R	T	G	U	W	M	W	T	B	R	I	F	L	K	M	K
D	R	M	K	I	X	F	I	A	M	V	B	T	H	P	T	H	A	R	J
K	L	B	K	L	I	L	H	O	C	H	R	H	P	K	E	E	K	M	R
T	R	I	Y	L	U	D	I	M	A	N	A	B	I	I	U	N	N	J	N
W	S	J	I	Y	W	N	B	Q	U	I	J	R	V	V	B	M	D	D	Z
M	X	D	N	N	I	C	H	G	H	S	X	N	Z	M	A	W	D	A	O
R	A	A	V	M	L	N	N	A	G	M	T	V	P	U	D	O	B	T	M
S	Y	P	A	M	P	I	R	Z	L	A	W	F	M	H	H	N	D	M	S
N	A	A	L	T	B	A	T	C	X	I	K	H	D	A	I	G	V	P	H
Y	W	H	W	M	J	M	H	M	T	L	M	K	U	M	R	O	L	Q	U
R	N	W	A	A	W	K	P	A	W	X	C	Q	Z	M	I	Z	N	A	K
L	C	M	H	B	F	V	B	R	J	U	R	P	U	A	F	O	M	X	U
L	M	S	Y	W	A	W	V	D	B	I	J	L	R	D	U	I	K	B	R
B	I	N	A	D	A	M	U	M	Z	N	R	I	I	P	T	H	Y	Y	A
K	H	I	F	A	D	H	I	T	D	T	L	A	Z	A	Y	Y	X	W	N
V	J	T	Z	H	V	U	K	R	I	S	T	O	Y	A	N	D	F	J	I
V	H	K	H	A	T	A	M	A	N	N	A	B	I	Y	Y	I	N	V	F
H	H	P	V	Y	N	G	K	M	S	A	M	A	H	A	T	C	G	N	N

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Ansarullah Wafanya Maonyesho Masjid Salaam

Kutoka uk. 1

ambapo tulimpatia Baiat akaisome kabla hajajiunga.

Bw. Hamisi Saburi skies ndani ya gari yake akisubiri taa za barabarani zimruhusu kwenda, baada ya kuiona Picha ya Masihi Aliyeahidiwa na alipouliza ni nani huyu mtu, akaambiwa ni Masihi Aliyeahidiwa au Yesu wa mfano, alipata shauku na kumpatia Mhudumu wetu namba Zake ili Tumpelekee vitabu vinavyoelezea juu ya Jamaat.

Alipelekewa vitabu ofisini Kwake na akanunua vitabu aina saba tofauti. Ameahidi kuifutilia jumuiya ili aijue.

Wanajamaat wengi wamevutiwa na maonesho hayo hususan mabango ya hoja na Picha ya Masih ambavyo vilikuwa vivutio kwa watu wengi.

Wako watu waliokasirishwa juu ya Madai au hoja walizofikishiwa, na wanadai sisi tumepotea njia na tunapotosha watu.

Maonesho yalifunguliwa na Muwakilishi wa Serikali ya Mtaa wa Mchafukoge ambaye Anavutiwa na Jumuiya yetu kwa juhudi Zake za kueneza dini kwa njia ya Amani. Alipewa zawadi ya vitabu na Alitoa shukuran kwa jumuiya kuweka maonyesho ya wazi ili watu wengi wajionee. baada ya ufunguzi wa maoneaho hayo Sheikh Shahab Sahib aliongoza maombi ili kupata Baraka na ridhaa za Allah.

Maonyesho yalifungwa tar 28 na Sadr Ansarullah na Maombi yaliongozwa na Bw Hemed Sheikh Ubwa.



Mmoja wa wapita njia akitazama vitabu katika banda la Maonyesho mbele ya Masjid Salaam



picha ya pamoja baada ya ufunguzi wa Maonesho ya vitabu

Sheikh wa Jumuiya Sheikh Khuram Shahzad baada ya kuona Mvuto wa watu katika maonyesho hayo hususan Picha kibwa ya Masihi Aliyeahidiwa watu wanavyovutiwa nayo, Alitoa maoni kuwa maonyesho ni mazuri na ikiwezekana yaendelee siku zote.

Kambi ya Malezi kwa Ansarullah

Majlis Ansarullah Mkoa wa Dar es Salaam iliendesha Darasa la malezi kwa kufanya kambi ya siku mbili toka tarehe 29 hadi 30 Juni.

Mada nne makhsusi ziliwasilishwa na wahadhri ambazo ni

(i) Ujasiliamali na Uchamungu
ii. Mazingatio ya Afya kwa Ansarullah
iii. Ansarullah tuache urithi gani kwa vizazi vyetu
iv. Islam na Utandawazi

Alhamdulillah kambi ilienda vizuri mno.

Jumla ya Ansarullah 103 walishiri kambi hiyo wakiwepo Ansarullah 7 Kutoka Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Nazim A'la Mkoa Huo Bwana Ramadhani Makunganya na Rais wa Mkoa Bwana Yusuf Malinda Sahib.

Katika kambi hiyo Lajna Imaillah walikuja kujitolea kwa ktupikia chakula siku ya Jumamosi usiku. Jazaakumullah Ahsanal jazaa. Allah Awalipe malipo Mema kabisa kwa ushirikiano waliotupatia.

Shukrani za dhati ziwafikie Majlis Khudamul Ahmadiyya. Tuliomba vijana Saba watuhudumie. Naaam, vijana hawa walionesha uhudumu hasa sawa na Lakabu Yao.



Sehemu ya washiriki wa Kambi ya Malezi ya Ansarullah 2019

Kutuandalia viti, kuleta chakula na kugawa kwa ustarabu na bashasha kabisa katika nyuso zao wakati wanatuhudumia, macho yalikuwa yanalengwa na machozi Kila na moyo kuwa na dukuduku kwa kupendezwa na kufurahishwa na jinsi wanavyojitolea, kutujali na kuonesha heshima kubwa kwetu. Allah Mtoaji wa malipo, Awalipe malipo yasiyo idadi. Amin

Hawa Khuddam, siku ya Jumamosi majira ya saa nne usiku wakati kibaridi kinachonyota miili yetu, Alhamdulillah!, Walikuja na chai ya Moto na kahawa, na vitafunwa karanga na Ndizi za *crops*, MashaAllah. Hakuna Ansar aliyelala, Wote tulichangamka na kuona kama saa Saba mchana.

Tunawashukuru sana tukianza na Sadr Khuddam na vijana uliotupatia:- Bw Musa Mgeleka Sahib, Musa Kayombo Sahib, Adam Makame Sahib, Ramadhani Abed Sahib , Sahaban Rajab Sahib na iwapo yuko niliyemsahau, Jazaakumullah Ahsanal Jazaa.

Shukrani ziwaendee Wote waliojitoale na kufanikisha shughuli hii waliokuwa katika Idara Mbalimbali Jazaakumullah Ahsanal Jazaa

Shukrani ziwafike Ansarullah Wote walichingia Mali kufanikisha zoezi hili . Allah Awalipe na Kuwajazia pale mlipotoa . Amin

Mwisho Shukrani za dhati ziwafikie Waandaaji na wasimamizi wakuu wa shughuli hii, Naib Sadr Sad Dom Bw. Akbar Kazema na Qaid Tarbiyya Bw. Fadhil Pazi. Allah Akulipeni kwa kusimamia na kuratibu shughuli yote kwa ufanisi. Jazaakumullah Ahsanal Jazaa

Inshallah wasaa ukipatikana, Tutaweka Muhtasari wa Mada zote ili na wengine wafaidike na Mafundisho yaliyotolewa.

Jazakumullah Ansarullah Wote Mlioshiriki kambi hii na wale waliotuombea kufanisha kambi hii.

Pia Allah Awatilie wepesi Ansarullah Wote waliomba ruhusa kwangu na kwa nazim Ala. Wameonesha mfano bora wa kujali wito japokuwa kwa Nashua mbalimbali hawakuweza kufika.

Mwisho sifa zote njema zinamstahiki Allah - Mola wa walimwengu.

MATUKIO KATIKA PICHA



Watoa mada katika kambi ya malezi ya Ansarullah



Kamati ya usimamiz wa ujenzi wa jengo la Ansarullah wakihamasisha na kukusanya michango katika msingi wa jengo hilo



Nasrat Ahmadiyya wakipokea zawadi za ushindi katika Ijtimaa ya Lajna Imaillah 2019



Banda la Ahmadiyya katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es salaam maarufu Sabasaba 2019



Mabango ya mahubiri katika maonyesho ya vitabu ya Ansarullah Masjid Salaam



Picha ya pamoja baada ya kumalizika kwa Ijtimaa ya kwanza ya Khuddamul Ahmadiyya Kanda ya Kaskazini iliyofanyika Kahama 2019



Mashindano ya Ijtimaa ya Atfal ul Ahmadiyya Tanzania 2019



Washiriki wa Ijtimaa ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania 2019 katika picha ya pamoja na Amir Jamaat Tanzania

Darasa La Qur'an Tukufu

MZIZI WA KILA MAASI NI UJINGA NA YAKIN NDIO JIBU

ٱللَّهُ ٱلَّذِى رَفَعَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ بِغَيۡرِ عَمَدٖ تَرَوۡنَهَا
ثُمَّ ٱسۡتَوَىٰ عَلَى ٱلۡعَرۡشِۖ وَسَخَّرَ ٱلشَّمۡسَ وَٱلۡقَمَرَۖ
كُلٌّ يَجۡرِى لِأَجَلٖ مُّسَمًّىۚ يُدَبِّرُ ٱلۡأَمۡرَ يُفَصِّلُ ٱلۡأٓيَٰتِ
لَعَلَّكُم بِلِقَآءِ رَبِّكُمۡ تُوقِنُونَ

Surah 13:3

Allah ndiye Aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona. Kisha Akastawi juu ya Arshi. Na Akavitiisha jua na mwezi; kila kimoja kinaendelea mpaka muda uliowekwa. Yeye Hulitengeneza (kila) jambo. Huzieleza Aya ili mpate yakini ya kukutana na Mola wenu.

YAKINI Ni Udhibitisho wa Ufahamu/Ujuzi. Ni Elimu inayohakiki juu ya Maarifa fulani.

Katika aya hii Allah Amejieleza katika Ustadi wake wa Uumbaji ili kujibambanua na Ajulikane. Na katika YAKINI ndimo Kufuata au Kutii au Ibada Inapopatikana, 30:27. Katika Yakini ndimo njia Iliyonyooka.

Seyidna Ahmad as amesema: "***Enyi watu mumtakao Mwenyezi Mungu! Fungueni masikio na msikie kuwa hapana kitu kama yakini. Yakini peke yake ndiyo humfungua mtu katika madhambi. Yakini ndiyo inayotoa uwezo wa kutenda mema. Na yakini ndiyo imfanyayo mtu ashiki na mpenzi hasa wa Mola wake. Je! mnaweza kuacha dhambi bila yakini? Mnaweza kujikataza matamanio ya nafsi zenu bila nuru ya yakini? Au mnaweza kupata utulivu wa roho bila yakini? Au mnaweza kujibadilisha kweli kweli bila yakini? Je, iko kafara au sadaka yo yote chini ya mbingu yenye kuweza kuwaondoleeni dhambi? Au je damu isiyokuwa ya asili ya Isa mwana wa Mariamu inaweza kuwaokoeni katika madhambi . . . ? Mtu huondolewa katika madhambi anapomjua kwa yakini Mwenyezi Mungu na uwezo Wake na malipo Yake.***

Hakika MZIZI WA KILA MAAASI NI UJINGA. Mwenye kupata sehemu ya maarifa ya Mungu kwa yakini hawezi kuendelea kumwasi. Mwenye nyumba hawezi kukaa nyumbani mwake akijua kwamba tufani la maji linakuja kwenye welekeo wa nyumba yake; au moto umezunguka nyumba yake na umeiunguza ila pamebakia pahali padogo tu. Basi huyu hawezi kungojea katika nyumba ile. Kwa nini ninyi mmekaa katika hali yenu yenye hatari baada ya kujidai kuwa mna yakini kwa malipo ya Mungu? Basi fumbueni macho yenu na tazameni hukumu za Mungu zilizomo duniani. Na msiwe mapanya waendao chini ya ardhi; bali kuweni njiwa warukao juu na kupenda hewa ya mbinguni. Jihadharini msifanye madhambi baada ya kutubia, wala msiwe kama nyoka mwenye kujichubua gamba lake na ni nyoka vile vile. Yakumbukeni mauti siku zote, kwani yanawasogeleeni pole pole, lakini ninyi mmeghafilika nayo. Jitahidini mtakasike, sababu mtu hawezi kumpata Mtakatifu (Mwenyezi Mungu) mpaka ajitakase mwenyewe. Lakini mnawezaje kupata neema hii? Mwenyezi Mungu amejibu Mwenyewe kama anavyosema katika Qur'an tukufu: Wasta 'iinuu bissabri wassalaat, yaani, Ombeni msaada kwa subira na kwa Sala" (sura 2:46) (Safina ya Nuhu).

Ndivyo ilivyo katika mambo mengine ufaulu wa jambo lolote lako linategemea yakini juu ya jambo hilo. Na yakini inapatikana kwa kuchunguza jambo chanzo chake na mpaka mwisho wake, jambo hilo limeshikiliwa na nini? au linatokana na nini au uwepo wake unategemea nini? n.k

Tunamuomba Allah Atujalie yakini iliyokamili juu ya utambuzi wake. Amin

Imeandaliwa na Musa Salum - 0717 504 690

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA

Kuwarehemu Ndugu

Ninyi hamuwezi kukubalika kwake hadi dhahiri yenu na batini yenu ziwe namna moja. Warehemuni wadogo juu ya kwamba m wakubwa, wala msiwahakirishe, mkiwa wenye Elimu, wapeni nasaha walio wajinga, wala msiwadhalilishe kwa kujivuna. Na mkiwa matajiri, wahudumieni walio masikini, sio kuwafanyia Kiburi kwa kujipenda. Ziogopeni njia za Maangamio. Dumuni kumuogopa Mwenyezi Mungu na mshikamane na Ucha Mungu, ... Ni mwenye bahati mbaya alioje Mtu yule asiyeyaamini Maneno haya yaliyotoka kinywani mwa Mwenyezi Mungu ambayo nimeyabainisha. Ikiwa mwataka Mwenyezi Mungu Awe radhi nanyi mbinguni, basi kuweni wamoja kama ndugu wawili waliotoka tumbo moja. Miongoni mwenu aliye mcha Mungu zaidi ni yule anayeyasamehe zaidi madhambi ya nduguye na mwenye bahati mbaya ni yule afanyaye ushupavu, asiyesamehe.

(Safina ya Nuhu, Ruhani Khazain, J. 19, uk 12 -13).

Kudhihiri kwa Masihi, Muokozi wa Walimwengu.

Na **Majlis Ansar Sultanul Qalam.**

Toka enzi ya Nabii Issa (a.s) au Yesu, Masihi Aliyeahidiwa aliotabiriwa kufika katika vitabu vitukufu. Wakristo wakimsubiri yesu aliyepaa mbinguni kurejea na kuisismamisha dunia dola ya kikristo na waislamu wakingojea Issa mwana wa maryam kurejea tena na kuivunja misalaba na kuushindisha uislam. Pole kwa wote wanaosubiri maana wao wameghafilika sana.

Ilishaandikwa katika danieli "na kutoka wakati ule kuendelea kwa sadaka za kuchomwa zitakapoondolewa na chuki za zile linalochukiza litengezwe, zitakuwa siku moja elfu mia mbili na tisini. Ana heri angojae, na kuwa siku moja elfu mia tatu na tano na siku siku thelathini. Wanazuoni wa kikristo walipiga hesabu juu ya ujaji wa masihi na ilitabiriwa afike miaka ya 1868, zaidi ya hapo Dr. Dumbleby (mwanachama wa British chronological and Astronomical Association) aliandika katika kitabu chake cha "nyakati zilizochaguliwa" kwamba haingezidi miaka ya 1898 kabla ya masihi kurudi tena duniani.



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as]
Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa

Cha ajabu na ni masikitiko makubwa kwa wale Wakristo wanaoendelea kungojea katika karne hii ya 20 (sasa 2019) wakimtaka yule yule yesu kurudipo duniani. Nasema tena, pole kwa wote wanaosubiri, maana wao wameghafirika sana.

Imeandikwa katika Qur'an (11:18) "basi je, mtu aliye na dalili wazi itokayo kwa Mola wake, na shahidi mmoja atokaye kwake atamfuata na kabla yake kulikuwa na kitabu cha Mussa kilichokuwa kingozi na rehema". Mtu aliye na dalili wazi, yaani Mtume (s.a.w) ambaye ukweli wake na ukweli wa mafundisho aliyoleta umethibitika. Shahidi mmoja atokaye kwake atamfuata; shahidi hutakiwa kwa ajili ya kuhakikisha jambo fulani. Wakati mafundisho ya Islam yamefanyiwa shaka hasa ni baada ya miaka 1350. Kuna baadhi ya Waislam wenyewe wanaofikiri mafundisho ya Qur'an, has ya sala ya tano za kila siku, kukata mikono ya wezi, kuoa wake zaidi ya mmoja, wanawake kufunika nyuso zao barabarani na wanawake kutochanganyika hovyo na wanaume wasio jamaa zao, riba n.k kwamba yanahitaji kubadilishwa. Kuna watu wanaofikiri kuwa sheria ya islam imetanguka, na wanataka kuleta sheria mpya mahala pake. Kuna hao wapinzani wa Ulaya na Amerika wanaodadisi usahihi wa baadhi ya mambo ya kihistoria yaliyotajwa na Qur'an na pia wakilaum kuwa mafunzo mengine ya Qur'an si mazuri kufuata. Mambo kama haya hayakupata kutokea kabla ya zama hizi na bila shaka kabla yake hapakuwa na haja ya shahidi.

Shahidi huyu aliyefika wakristo na waislam wote sikilizeni, ni mjumbe wa mwenyezi mungu, seyyidna Ahmad, Masih na Mahdi Aliyeahidiwa, ambaye alianzisha Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya baada ya mafundisho ya islam yalipokataliwa na watu wazi wazi.

Ni yeye aliyefika kabla ya 1898 kama nukuu zilivyomuhitaji, yeye alizaliwa 1835 na kutangaza kuwa yeye ndiye yule Aliyeahidiwa miaka ya 1981 na vitabu vitukufu. Hakuna bishara, katika vitabu vitukufu ambayo humpinga dai lake. Yeye ndiye aliyeletwa kama yesu na Issa wa mfano katika dunia yetu. "wote tumtolee salamu na kufungamana naye". Hii ndiyo njia pekee ya kuulinda ulimwengu wetu. Mungu atujaalie kumtambua na kumkubali Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s).

Miadi niknayotia, enyi watu wachunguzi
Subirirni kutimia, mfanye upelelezi
Kama haikutimia, mnifanye mpuuzi
Kiukeni kuta hizi, muingie mwangu nyumbani.

Hadhrat Zaid Bin Harith ra

Inatoka uk 12

kama wewe ni mjumbe wa Mungu kweli basi hakuna katika watu hawa watatu atakayerudi hai kwa sababu neno lolote linalotamkwa na nabii ni lazima litimie. Hekima ya Mwenyezi Mungu ikaamua hivyo kwamba tukio hili litimie hasa kwa njia hiyo. Hadhrat Zaid[ra] aliuawa. Kisha, Hadhrat Ja'afar[ra] akachukua uongozi wa jeshi. Naye pia akapata ushahidi. Kisha, Hadhrat Abdullah bin Rawaha[ra] akachukua uongozi wa jeshi naye pia akapata ushahidi. Ilikuwa karibu fadhaa isambae miongoni mwa wanajeshi lakini Hazrat Khalid bin Waleed[ra] alichukua bendera mkononi mwake kwa kuwaongoza Waislamu. Allah alitoa ushindi kwa Waislamu kupitia yeye na alirudi na jeshi salama.

"Katika wakati wa kifo chake, Hadhrat Zaid[ra] alikuwa na umri wa miaka hamsini na tano. Mtume[sa] aliongoza sala ya jeneza ya Hadhrat Zaid[ra] na kusema kuwa "Enyi watu! Muombeeni maghfira Zaid, kwani yeye kwa wepesi ameingia kwenye makazi ya peponi. "

Hazrat Jabala anasimulia kwamba mpaka pale Mtume[sa] alipotoka kwa ajili ya vita, hakuwahipo kutoa silaha yake kumpatia mtu yeyote isipokuwa Hadhrat Ali[ra] na Hadhrat Zaid[ra]. Hazrat Jabala anasimulia mahala pengine kwamba Mtume[sa] alipewa matandiko ya ngamia wawili kama zawadi. Moja akaliweka kwa ajili yake mwenyewe na lingine akalitoa kumpatia Hadhrat Zaid[ra]. Kisha, Hazrat Jabala anasimulia tena kuwa Mtume[sa] aliwahi kupewa makoti mawili. Moja akaliweka kwa ajili yake mwenyewe na lingine akampatia Hadhrat Zaid[ra].

Kiini cha kile ambacho vitabu vya historia vimeeleza kuhusu vita vya Mu'tah ni kwamba kwa ajili ya kukabiliana na vita ya Mu'tah, Mtukufu Mtume[sa] alitayarisha jeshi kubwa katika mwezi wa Safar katika mwaka wa 11 AH, na katika mwezi huu huu kwenye mwaka wa 11 AH, Mtukufu Mtume[sa] aliwaagiza watu kujiandaa kwa ajili ya vita dhidi ya Roma. Siku moja baada ya jeshi hili kuwa tayari, Mtukufu Mtume[sa] alimwita Hazrat Usama bin Zaid[ra], na, kuukabidhi uongozi wa safari hii kwa Hadhrat Usama[ra], na akasema, "Nenda upande wa mahali ambapo baba yako aliuawa, "na, kuhusu kuondoka kwao kuelekea taifa la Syria, Mtume[sa] alisema," Wakati wa wewe kuondoka, usafiri kwa haraka sana na kumfikia adui kabla habari ya kwenda huko kuwafikia. Kisha, jambo la kwanza asubuhi, muwashambulie watu wa Balqa (Ahl-e-Ubna). "Mtume[sa] akaliagiza jeshi kwamba,"Yaangusheni maeneo haya chini kwa farasi wenu, kwa kulipiza kisasi cha Hadhrat Zaid."

Mtume[sa] akazidi kumweleza Usamah, "Chukua waongozaji ambao wanaweza kukuonyesha njia, na pia chukua watu wale ambao wanaweza kufanya wajibu wa upelelezi - watu ambao wanaweza kukupatia taarifa vizuri juu ya hali ya mambo ilivyo huko. Mwenyezi Mungu Akupe mafanikio na kurudi haraka.

"Wakati wa vita hivi, umri wa Hazrat Usama ulikuwa kati ya miaka 17 na 20. Mtume[sa] alifunga bendera kwa mikono yake mwenyewe na kumwambia Usamah, "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, jitahidi katika njia Yake, na pigana vita na yule ambaye anayemkanusha Mungu." Baadhi ya watu walileta upinzani kwamba kijana ambaye amefanywa Ameer alikuwa na umri mdogo juu ya masahaba ambao wamehama pamoja na Mtume[sa] katika kipindi cha mwanzoni sana mwa Uislamu. Wakati huu, Mtume wa Allah akahuzunika sana. Yeye alisimama kwenye mimbari na kutangaza, "Enyi watu, ni mambo gani haya ya ajabu yaliyonifikia mimi ambayo mnasema kuhusu Usamah (kufanywa) Kiongozi kati yenu? Kama mnanipinga kumfanya Usama Ameer juu yenu, basi eleweni kwamba ninyi mlishayapinga maamuzi yangu ya kumfanya baba yake kuwa Ameer juu yenu kabla hili. Naapa kwa Mungu, yeye alikuwa na sifa za uongozi, (akimaanisha Hadhrat Zaid bin Harithah) na baada yake, mwanawe pia anazo ndani yake sifa za uongozi. Yeye alikuwa miongoni mwa watu ambao walikuwa wapendwa kwangu, na wote hawa (yaani baba na mwana) wanastahili mazuri yote katika dunia."

Cha kusikitisha, Mtume[sa] akawa mgonjwa sana mara baada ya hapo na akafariki siku ya Jumatatu 12 Rabi-al-Awwal, baada ya jua kutua. Baada ya kufariki Mtume[sa], fitna na kuritadi vikaenea kote Arabia nzima. Waislamu walikuwa katika hali mbaya sana. Masahaba wakubwa wakapendekeza kwa Hazrat Abu Bakr[ra] kwamba kutokana na hali kuwa mbaya, lazima acheleweshe kupeleka jeshi la Hazrat Usama[ra] na kwamba linapaswa kutumwa muda mwingine baadaye. Hazrat Abu Bakr[ra] alikataa, na kusema kuwa hata kama wanyama watavuta mwili wake kwa kuuburura, atalituma jeshi hili kwa mujibu wa maelekezo ya Mtukufu Mtume[sa] na yeye atatekeleza maelekezo aliyopewa na Mtume[sa]. Hazrat Abu Bakr[ra] akaendelea kushikilia uamuzi wa Mtukufu Mtume[sa] na akalipeleka jeshi kwenye safari hii kama ilivyoagizwa na Mtukufu Mtume[sa].

Hazrat Abu Bakr[ra] aliuhitaji msaada wa Hazrat Umar[ra] katika Madina kwa ajili ya masuala kadhaa. Hata hivyo, Hazrat Abu Bakr[ra] hakumbakisha Hazrat Umar[ra] nyuma kwa hiari yake mwenyewe. Badala yake alitaka ruhusa kutoka kwa Hazrat Usama[ra] kama anadhani ni sawa kumruhusu Hazrat Umar[ra] kubaki nyuma. Hazrat Usama[ra] aliitikia wito wa Khalifa na kumruhusu Hazrat Umar[ra] kubaki nyuma (Madina).

Mwishowe, Hazrat Abu Bakr[ra] alitoa maneno yafuatayo ya ushauri kwa jeshi: "Msionyeshe utovu wa utiifu wala msivunje maagano yenu, wala msiibe, wala msiiharibu maiti yoyote ya adui, msiwauwe watoto wadogo, wanawake na wazee; wala msikate miti ya mitende wala msiichome moto, wala msimdhuru kondoo yoyote, ng'ombe au ngamia isipokuwa kwa wale mtakaowachinja kwa ajili ya matumizi ya chakula "Kisha akaendelea kusema:". Ninyi mtakutana na watu ambao wamejitenga Makanisani kwa ajili ya ibada, waacheni hao. Vile vile, kutakuwa na watu ambao watakuleteeni chakula katika vyombo vyao. Mkitaka mle humo, mnapaswa kutamka Bismillah [Kwa jina la Allah] kabla ya kula. Na bila ya shaka mtakukutana na watu ambao wananyoa vichwa vyao kutoka katikati, lakini watakuwa na mafungu ya nywele juu ya pande zote. Kwa ajili yao mnapaswa kuwagonga kidogo kwa panga zenu na kisha mjilinde... Namuomba Mwenyezi Mungu, Akulindeni na kashfa zote na Akulindeni nyote dhidi ya janga la tauni. "Hazrat Abu Bakr[ra] kisha akamgeukia Hazrat Usama[ra] na akasema: "Tekeleza majukumu yote uliyopewa na Mtume[sa]. "

Kwa njia ya mazungumzo haya, wakati kwa upande mmoja Hazrat Abu Bakr[ra] alimfundisha Hazrat Usama adabu ya Kiislamu juu ya vita - ambapo mtu hawezi kufanya udhalimu dhidi ya mtu mwingine - kwa upande mwingine pia ni dhahiri kwamba Hazrat Abu Bakr[ra] alikuwa anaamini kuwa jeshi hili litapata ushindi. Hii ndiyo sababu alisema: ".Ninyi mtapewa ushindi" Baadaye, kwenye safari hii jeshi hili lilipata mafanikio makubwa, hakuna mpiganaji Muislam hata mmoja aliyeuawa, na Waislamu wakapata kiasi kikubwa cha ngawira za vita, ambapo sehemu moja ya tano ikatengwa pembeni na iliyobakia ikagawanywa miongoni mwa wanajeshi. Kwa wale waliokuwa na kipando wakapata mara mbili ya wale waliotembea kwa miguu. Baada ya vita, jeshi likapiga kambi katika eneo hili hili kwa siku moja na kisha likaondoka kwenda Madina siku iliyofuata. Yalikuwa ni maamuzi magumu na ya ujasiri mkubwa kwa Khalifa kutuma jeshi hili, licha ya hatari kadhaa za ndani na nje pamoja na masingizio fulani. Kisha kupitia ushindi na mafanikio, Mwenyezi Mungu akawafundisha Waislamu somo lao la Kwanza kwamba baada ya kufariki Mtume[sa], baraka zote zimo katika kuutii Ukhalifa.

Baada ya Swala ya Ijumaa, nitasalisha sala mbili za jeneza ya ghaib. Sala ya jeneza ya kwanza ni ya Siddique Adam Dambia Sahib, ambaye alikuwa Mbashiri akihudumia katika Ivory Coast. Alikuwa mgonjwa kwa muda kabisa na hivi karibuni afya yake ilidhoofika zaidi na hatimaye kupelekwa Hospitali ya Jeshi, ambapo alifariki tarehe 14 Juni, Innaa Lillaahi wainna Ilayhi raajiuun. Siddique Adam sahib alizaliwa Lausangeh, kijiji kimoja katika Ivory Coast, mwaka 1950. Alipokea Ahmadiyya muda mfupi kabla ya 1977. Mbali na mke wake, ameacha mabinti 7 na wana wa kiume 2. Baada ya kujitolea maisha yake kwa ajili ya huduma ya Jamaat katika 1981, alisafiri kwenda Pakistan kwa miguu akifuatana na rafiki wengine mawili. Walisafiri kwa takriban mwaka 1 mzima na kukabiliana na matatizo mengi ya safari, hatimae waliwasili Rabwah mwaka 1982 na kuanza kusoma katika Jamia Ahmadiyya. Yeye alimaliza masomo yake katika 1985-1986 na kisha akarudi Ivory Coast. Hadi kifo chake, alikuwa ametumika kama mbashiri katika nchi mbalimbali za Afrika Magharibi kwa kipindi cha zaidi ya miaka 30. Mtindo wa Siddique Adam Sahib wa utoaji hotuba ulikuwa wa kuvutia sana kwa wenyeji wanaozungumza lugha ya asili, Jula. Alikuwa pia anaendesha vipindi kwenye redio. Vipindi hivi vilikuwa vya ubora wa hali ya juu sana na vilikuwa maarufu sana. Mwenyezi Mungu, Amruzuku msamaha Wake na rehema na kuinua cheo chake. Pia Mwenyezi Mungu Awape watoto wake uvumilivu na subira na kuwawezesha kuendeleza matendo yake mazuri.

Sala ya Jeneza ya pili ni ya Mia Ghulam Mustafa Sahib Mirak kutoka wilaya ya Okara. Alifariki dunia tarehe 24 Juni, katika umri wa miaka 83 - Innaa Lillaahi wainna Ilayhi raajiuun. Marehemu alikuwa Ahmadiya wa kuzaliwa na alikuwa na shauku kubwa kwa ajili ya kuabudu.

Alikuwa anashiriki kwenye Sala za jamaa kwa kudumu pamoja na kusali sala ya Tahajjud, na alikuwa mtoaji wa Adhana ya sala ya Alfajiri katika eneo lake. Daima alikuwa akiwaamsha wanafamilia yake kwa ajili ya sala ya Alfajiri na Mwenyezi Mungu alimpa uwezo wa kufunga saumu ya Ramadhan hadi kufariki kwake. Alikuwa na hamu kubwa kwa ajili ya Tabligh na daima kwa njia moja au nyingine alikuwa akifikisha ujumbe wa Ahmadiya kwa kila mtu aliyekutana naye. Alikuwa mtu mwenye ukaribu sana na watu, mtu mwema na mkweli. Alikuwa na mahusiano makubwa ya upendo kwa Ukhalifa na mara kwa mara alikuwa akisikiliza hotuba za Ijumaa na kuwafanya watoto wake kusikiliza pia. Mungu Mwenyezi, Amjaalie rehema na msamaha na kuinua cheo chake. Ghulam Murtaza Sahib (mtoto wake), ambaye ni mbashiri, yuko mbali na nyumbani kwao akishughulika na kufikisha ujumbe wa Mweneyzi Mungu na kama nilivyosema hataweza kurudi nyumbani kwa mazishi. Mwenyezi Mungu, Amruzuku uvumilivu na uthabiti wa kubeba hasara hii. Baada ya Sala ya Ijumaa, Inshallah, nitasalisha Sala za jeneza ghaibu.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SHAW. - DH. QA'D 1439 AH | JULAI 2019 | WAFA 1398 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Kama kila wakati mtazingatia kujiepusha na hasira basi Husuda na kinyongo vyevyewe vitatoweka. Yeyote kati yenu ashikwapo na hasira na hali amesimama, basi aketi chini, kama hasira ikiondoka kwa njia hiyo basi ni vyema waila alale chini. (Musnad Ahmad bin Hambal, J.5, uk. 152, Chapa ya Beirut).

Hadhrat Zaid Bin Harith^{ra}

Katika hotuba ya tarehe 28/06/2019, baada ya Tashahhud, Taawwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Momeneen, Mirza Masroor Ahmad^{atba} alisema:

Kuna simulizi chache kumhusu Hazrat Zaid bin Harithah^{ra} ambazo nitazisimulia leo.

Mnamo mwezi wa Rabi-ul-Akhir mwaka wa 6 A.H, Mtume mtukufu saw aliwatuma Waislamu wachache kwenda katika kabila la Bani Sulaim chini ya uongozi wa mtumwa aliyemwacha huru ambaye hapo kabla alimpanga kuwa mwanawe; Hadhrat Zaid bin Harithah^{ra}. Kabila hili lilikuwa linaishi katika mkoa wa Najd katika mahala panapoitwa Jamum na lilikuwa limo vitani dhidi ya Mtume saw kwa kipindi fulani hadi wakati huo. Kwa hakika kabila hili lilitoa mchango mkubwa dhidi ya Waislamu katika Vita vya Handaki pia.

Wakati Zaid bin Harithah^{ra} na wenzake walipofika Jamum, ambayo ilikuwa iko umbali wa takriban maili 50 kutoka Madina, walikuta hakuna mtu. Hata hivyo, walipata kujua sehemu ambayo baadhi watu wa kabila la Bani Sulaim walikuwepo. Kwa kutumia mbinu za kiuchunguzi, Zaid bin Harithah^{ra} akawashambulia mahala ambapo walikuwa wanalisha mifugo yao. Mashambulizi haya ya ghafla yalipelekea watu wengi kukimbia na kutawanyika hapa na pale. Hata hivyo, Waislamu waliweza kukamata wafungwa wachache na baadhi ya mifugo, ambayo walibeba na kisha kurudi Madina.

Hazikupita siku nyingi tangu kurudi kwa Zaid bin Harithah^{ra}, wakati Mtukufu Mtume^{sa} alipomtuma kutoka Madina kwa mara nyingine tena katika mwezi wa Jamadi'ul-Ula, akiongoza kikosi cha wenzake 170 ili kukabiliana na msafara wa Makureishi uliokuwa unawasili



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba ya Ijumaa kwa waaminio na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

kutoka Syria. Ni muhimu kuelewa sababu, ni kwa nini misafara huu ulitekwa. Hii misafara ya Makuraishi ilikuwa daima inabeba silaha wakati kusafiri kati ya Makka na Syria na wao walikuwa hupita karibu sana na Madina, hivyo kulikuwa na tishio mara kwa mara. Pia, watu wa misafara hii walikuwa wakiyashawishi makabila ya Arabia yasimame dhidi ya Waislamu popote walipokuwa wakipita. Kutokana na hili, moto wa hatari wa kujenga uadui juu ya Waislamu ulikuwa umewashwa nchini kote. Hadhrat Zaid bin Harithah^{ra} aliweza kufanikiwa kuifikia sehemu inayoitwa Is na kuuteka msafara, ambao ulikimbia kwa haraka. Zaid^{ra} aliteka wafungwa wachache na kuushika mzigo wa msafara akaubeba kuelekea Madina na kuwasili mbele ya Mtume^{sa}.

Ni lazima ikumbukwe kwamba misafara hii (ya Waislamu) haikuwa ya uchokozi, bali ilikuwa inafanyika tu kutegemea taarifa za kuaminika za kiusalama zilizopatikana juu ya hatari na njama za kuwashambulia Waislam katika Madina.

Hadhrat Zaid bin Harithah^{ra} alitumwa katika safari nyingine ya Tarif, lakini kabla ya Zaid bin Harithah^{ra} kuweza kufika huko, watu wa kabila hili walipata taarifa na kutawanyika. Baada ya muda mfupi wa kusubiri kwa siku chache, Zaid bin Harithah^{ra} na wenzake wakarudi Madina. Mara hii hakukuwa na vita yoyote iliyofanyika na wala hawakwenda zaidi kuwatafuta.

Kisha kuna safari nyingine ya Hadhrat Zaid bin Harithah^{ra} kuelekea eneo la Hisma, ambayo ilifanyika katika Jamadi-ul-Akhir 6 AH. Wakati wa safari hii, baadhi ya watu wa kabila fulani pia waliuawa ambao walikuwa wamesaini mkataba wa amani na Waislamu na kuukubali Uislamu. Hii ilitokea kwa sababu Zaid^{ra} alikuwa hana ufahamu juu ya mkataba huu. Mtume^{sa} mara kwa mara alionyesha huzuni yake kwa watu ambao waliuawa katika tukio hili na kuamuru kwamba wafungwa hawa lazima wapewe uhuru na ngawira za vita zirejeshwe. Baada ya kupokea agizo hili, Zaid^{ra} mara moja akafanya sawa na alivyoagizwa. Hivyo, huu ulikuwa mfano mwema kabisa wa Mtume^{sa} kuhusiana na kuheshimu ahadi zake. Inawezekana kwamba baadhi ya makabila kwa makusudi yalishiriki katika vita lakini kwa kuwa hili lilitokana na kutokufahamu kwa upande wa Waislamu, kwa hiyo, Mtume^{sa} aliwaachia huru wote na kuwarudishia mali zao.

Mapigano ya Mu'tah yalifanyika katika mwaka wa 8 AH. Mu'tah ni mahali karibu na Balqa katika Syria. Harith Bin 'Umair ra, ambaye alikuwa sehemu ya ujumbe wa Uislamu na alikuwa amebeba barua ya mtume s.a.w. kwa mfalme wa Basra, aliuawa katika eneo la Mu'tah. Tukio hili lilimuhuzunisha sana Mtume^{sa}. Wakati alipowaita watu, ambao idadi yao yafikia 3000, wao mara moja walikusanyika katika Jurf. Mtume^{sa} alitangaza kuwa Zaid Bin Harithah^{ra} atakuwa kiongozi juu ya wote. Yeye akatayarisha bendera nyeupe na kumpatia Hadhrat Zaid^{ra} na maelekezo yake, "Nenda hadi mahali ambapo Harith Bin 'Umair aliuawa na kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu hao. Kama watakubali, basi hilo ni jema na zuri kwao. Vinginevyo, ombeni msaada wa Allah dhidi yao na kupigana nao."

Mapigano ya Mu'tah yalitokea katika mwaka wa 8 AH, wakati wa mwezi wa Jamadul Awwal. Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah Bin Umar kuwa, "Mtume^{sa} alimteua Zaid bin Harithah^{ra} kuwa kamanda wa jeshi wakati wa vita ya Mu'tah na akasema, 'Kama Zaid atapata ushahidi (yaani atauwawa katika vita), basi Ja'far achukue nafasi yake, na kama Ja'far atapata ushahidi, 'Abdullah bin Rawaha achukue nafasi yake.' "Jeshi hili pia huitwa" Jaishul Umaraa "[Jeshi la Makamanda]. Baada ya kusema maneno haya, Myahudi mmoja aliyekuwepo katika tukio hili, akasema, 'Pamoja na kwamba mimi siamini kuwa wewe ni mjumbe wa Mungu, lakini

Endelea uk. 11

MABADILIKO YA MASAFA YA MTA AFRICA

'Frequency' ya sasa ni 12034

'Symbol Rate' ya sasa ni 27500

'Polarization' ya sasa ni H

Weka mabadiliko haya katika king'amuzi chako.

- Hakuna mabadiliko yoyote katika Satelaiti ambayo ni SES 5, 5° East
- Wala hakuna mabadiliko katika uelekeo wa dishi/ungo wako

Poleni kwa usumbufu utakaojitokeza.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com